**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

## HALMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA

Simu: +255 (026) 2650019 (G/L)
+255 (026) 2650021 (D/L)
Nukushi: +255 (026) 2650242
Barua pepe: ded@igungadc.go.tz
Tovuti: http://www.igungadc.go.tz

Halmashauri ya Wilaya
16 Mtaa wa Bomani,
45682 Igunga Urban,
S.L.P 19,
**IGUNGA.**

*Unapojibu tafadhali taja*
Kumb. Na. AB.285/294/01/78

27 Oktoba, 2025.

## TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA MWENYEKITI WA BODI YA AJIRA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga anawatangazia watu wote wenye sifa kuomba kazi ya nafasi ya Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira

### A. SIFA ZA MWOMBAJI

1. Awe raia wa Tanzania
2. Awe mkazi wa Halmashauri ya Igunga
3. Awe Mstaafu Serikalini
4. Awe hajawahi kushtakiwa na kosa lolote la Jinai
5. Awe na Umri kuanzia miaka 55 hadi 65 (sitini na tano)
6. Awe na Elimu ya Form IV au Form VI
7. Awe na Taaluma ya kuanzia Stashahada ya Juu /Shahada katika fani ya Sayansi ya Jamii katika Sheria, Utawala, Usimamizi wa Rasilimaliwatu au Uhasibu

### B. KAZI/MAJUKUMU

1. Kuendesha/kuongoza vikao vya Usaili wa waombaji wa nafasi za kazi
2. Kuendesha/kuongoza vikao vya kuwathibitisha watumishi kazini
3. Kuongoza /kuendesha vikao vya kupandisha /kuwabadilisha Watumishi vyeo

### C. POSHO

Kazi hii **haina Mshahara kwa kila mwezi**. Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira atakuwa analipwa posho kutokana na vikao vinavyokaliwa na Bodi

### D. MASHARTI YA JUMLA

1. Mwombaji aambatanishe Wasifu wake kwenye barua yake ya Maombi
2. Mwombaji aambatanishe nakala halisi ya vyeti vyake vya elimu na taaluma
3. Kila mwombaji aambatanishe picha 2 za pasipoti katika maombi yake

Maombi yote yatumwe kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga kuanzia tarehe **27 Oktoba,2025** hadi **10 Novemba,2025** Saa **9 :30** Alasiri

- Anwani ya kutuma

  **Mkurugenzi Mtendaji (W)**

  **Halmashauri ya Wilaya ya Igunga**

  **S.L.P 19**

  **45682 IGUNGA - MJINI**

Selwa A. Hamid

**MKURUGENZI MTENDAJI**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA IGUNGA